HOTUBA YA KATIBU MKUU WA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO, BW. SETHI KAMUHANDA KWENYE MKUTANO WA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MAENDELEO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MKURABITA ULIOFANYIKA COURT YARD HOTEL, DAR ES SALAAM, TAREHE 21 OKTOBA, 2010

Mratibu wa Mpango wa Kurasilimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Eng. Ladislaus Salema;

Wajumbe wa Bodi ya MKURABITA,

Wajumbe wa Mkutano,

Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe, Eng. Salema, kwa kunialika. Nimefarijika sana kwa kupata nafasi hii adhimu ya kuja kushiriki nanyi katika mkutano huu leo. Faraja yangu inatokana na ukweli kwamba ajenda ya mkutano huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wetu na nchi yetu. Hivyo, najiona ni mtu mwenye bahati kubwa. Nawashukuruni sana kwa heshima hii mliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Ndugu Wajumbe,

Vyombo vya habari vina wajibu na mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Wajibu huo ni pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa na huduma za kiuchumi mbalimbali zilizopo nchini ili waweze kuzitumia katika kujiletea maendeleo. Hii ni moja ya majukumu ya msingi ya vyombo vya habari duniani kote.

Kwani kama tunavyofahamu kazi ya uandishi wa habari duniani ilianza kwa kuandika habari za kibiashara. Mabepari wa Ulaya walioasisi uandishi wa habari kama tunavyoujua leo walianza kwa kuchapisha vijarida nilivyoelezea fursa za kibiashara zilizoko kwenye maeneo mbalimbali hususani kwenye makoloni waliyokuwa wanayatawala. Habari za kiasiasa zilianza kuandikwa baada ya muda mrefu kupita kwa lengo la kuhakikisha kwamba ubepari unaendelea kushamiri duniani.

Lakini tukiangalia hapa kwetu, vyombo vyetu vya habari bado vimejikita zaidi katika uandishi na utangazaji wa habari za kisiasa. Habari za kibiashara na kiuchumi hazijapewa uzito na umuhimu unaostahili. Lazima tufike mahali habari za kiuchumi nazo zianze kupewa kipaumbele katika vyombo vyetu vya habari. Na wakati huo ni sasa. Na mahali pa kuanzia ni kwenye Mpango wa MKURABITA.

Ni kwa msingi huo basi nimefurahi kusikia kwamba lengo la mkutano huu ni kuwapa fursa Waandishi wa Habari ya kubadilishana mawazo kuhusu Mpango wa MKURABITA ili kuwajengea uwezo wa kuwaelimisha Watanzania juu ya umuhimu wa mpango huu. Huu ni mwanzo mzuri. Naupongeza uongozi wa MKURABITA kwa uamuzi huu adhimu.

Ni jambo lililo dhahiri kuwa Waandishi wa Habari tunao wajibu mkubwa katika kufanikisha malengo ya MKURABITA. Na ili tuweze kutekeleza wajibu huo kwa mafanikio nawaomba tufanye mambo yafuatayo:

- Kwanza, sisi wenyewe kama waandishi wa Habari hatuna budi kuufahamu vizuri mpango wa MKURABITA. Inatubidi tujue chimbuko lake, malengo yake na madhumuni yake.

Inatubidi pia tujue hatua iliyokwisha fikiwa katika utekelezaji wa mpango huu na changamoto zilizopo. Nimeambiwa hili ndilo hasa lengo la mkutano huu wa leo. Naomba tulifanikishe.

- Pili, baada ya kuelewa mpango wa MKURABITA ni wajibu wetu kama Waandishi wa Habari kuutangaza ili ueleweke vizuri kwa kila mwananchi, aliyeko vijijini na mijini. Hili ni jukumu muhimu sana kwani mafanikio ya mpango huu yanategemea, ni kwa kiasi gani wananchi na hasa wale walioko kwenye sekta isiyo rasmi, wanaelewa fursa na faida za mpango huu. Na wenye uwezo wa kuwawezesha kupata uelewa huo ni sisi Waandishi wa Habari, mmoja mmoja na kwa ujumla wetu.

- Tatu, tunao pia wajibu wa kuibua majadiliano na mijadala kwenye vyombo vya habari kuhusu mpango huu. Hivyo ninawatarajia baada ya mkutano huu wa leo mtarejea kwenye sehemu zenu za kazi na kuanzisha mijadala rasmi kuhusu faida za MKURABITA katika kuboresha maisha ya Mtanzania na kukuza uchumi wa nchi yetu.

- Nne, mbali na mijadala nawatarajia pia mwende kwa walengwa wa MKURABITA kwa lengo la kupata mawazo yao na matarajio yao kuhusu mapango huu. Nimeelezwa kwamba walengwa wengi tayari wameukaribisha kwa furaha kubwa Mpango huu na wanayo matarajio makubwa ya mafanikio. Hivyo ni muhimu kwetu sisi kupata maoni yao na kuyaeleza ili iwe chachu ya kuwashawishi Watanzania wengine kushiriki katika MKURABITA. Hii pia itawapeni ninyi fursa ya kujua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa mpango na kushauri kuhusu namna bora ya kuzikabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Ndugu Wajumbe,

Moja ya madhumuni ya MKURABITA ni kuwawezesha wakulima kupata hati za kumiliki ardhi kwa ajili ya kuzitumia kama mtaji. Hali hiyo itawawezesha wakulima wetu kutumia ardhi yao kwa kukopa fedha za kuendeleza kilimo na shughuli zingine na hivyo kubadilisha maisha yao.

Aidha, baadhi yenu mnazo taarifa za nchi mbalimbali kuhusu faida zinazotokana na uwekezaji kwenye ardhi ambayo umiliki wake tayari umerasimishwa. Naomba tuibue mijadala kuhusu hili nalo ili wananchi wetu waone faida zitakazotokana na hatua ya Serikali ya kurasimisha umiliki wa ardhi hapa nchini. Tungependa wananchi walio wengi wachangamkie fursa hizo mapema ili tuanze kuona matunda ya mpango huu hasa katika maeneo ya vijijini wanakoishi wananchi wetu wengi.

Lakini naomba tusiishie hapo. Tuanze pia kuwaelimisha Watanzania ili waondoe hofu ya kukopa fedha kutoka kwenye Mabenki. Hivi sasa wengi wetu hatuna utamaduni wa kukopa kutoka taasisi za kifedha. Hali hii kwa kiwango kikubwa imerudisha nyuma kasi ya maendeleo yetu.

Sote tunaelewa kwamba watu wengi duniani wamepata mafanikio na maendeleo kupitia mikopo. Wameweza kujenga nyumba bora za kuishi, kuwapa watoto wao elimu bora na kuendesha magari mazuri kupitia mikopo ya mabenki. Naamini wakati sasa umefika nasi tuige mfano huo kwa kuondokana na woga wa kukopa. Na katika hili vyombo vya habari vina wajibu mkubwa. Naomba kazi hiyo tuianze sasa kupitia dhima ya Mpango wa MKURABITA. Tusisubiri tena.

Sanjari na hilo, tuanze pia kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa mikopo ya nyumba. Upatikanaji wa elimu hiyo

utawawezesha Watanzania wengi kujitokeza kukopa kwa ajili ya kujenga nyumba bora na za kisasa. Kama sote tunavyofahamu maisha bora ya mwanadamu ni pamoja na kuwa na nyumba bora ya kuishi. Na katika hili tayari Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisheria ya kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya nyumba. Kinachokosekana sasa ni elimu kwa wananchi. Naomba tushiriki katika kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari mnaviwakilisha hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nimefurahi sana kusikia kwamba uongozi wa MKURABITA umeandaa utaratibu wa kushirikisha vyombo vya habari kwa karibu zaidi katika shughuli zake kama ulivyofanya leo. Naomba utaratibu huo uwe wa kudumu kwani bado tunayo kazi kubwa ya kuwaelimisha Watanzania juu ya faida ya mpango huu ili waweze kushiriki kwa ukamilifu. Nadiriki kusema kwamba mafanikio ya haraka ya MKURABITA yanategemea sana ushirikiano kati ya uongozi wa Mpango na vyombo vya habari.

Hivyo ni matarajio yangu kuwa Waandishi wa Habari tutafanya kazi bega kwa bega na uongozi wa Mkurabita ili kuhakikisha kwamba mpango huu unafanikiwa kama ilivyokusudiwa. Naombeni hili liwe ndio azimio la mkutano huu. Tuondoke hapa tukiwa tumeazimia kufanikisha MKURABITA ili kuharakisha maendeleo ya watu wetu na nchi yetu.

Mwisho, napenda kutumia fursa hii kuupongeza uongozi wa MKURABITA kwa kushika nafasi ya pili katika Tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2010. Ushindi huu mnono umeiletea sifa na heshima kubwa nchi yetu kimataifa. **Hongereni sana.**

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Ndugu Wajumbe wa Mikutano,
Mabibi na Mabwana,

Baada ya kusema haya machache, sasa ninayo heshima ya kutamka rasmi kuwa mkutano huu umefunguliwa rasmi. Nawatakia nyote mkutano mwema wenye mafanikio.

Asanteni.